**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO**

Namba za Simu:

Mkuu wa Shule: 0786023421

Makamu Mkuu wa Shule: 0768711155
Mwalimu wa Taaluma: 0763681968
Email:
naisinyaihighschool2006@gmail.com

Shule ya Sekondari

Naisinyai,

S.L.P 5081,

**Mirerani**.

23.04.2023.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………

S.L.P……………………………………

…………………………………………

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NAISINYAI KIDATO CHA TANO 2023/2024 HALMASHAURI YA SIMANJIRO - MANYARA

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023, Tahasusi ya HGK. Shule ya sekondari Naisinyai ipo Mkoa wa Manyara, Halmashauri ya wilaya ya Simanjiro. Shule ipo umbali wa kilometa ishirini (20) toka kituo cha mabasi KIA. Kituo hiki kipo katikati ya mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha ambapo utapanda Hiace zinazoelekea Mererani na kushukia kituo cha Samaksi nauli ni shilingi 1,500/= hapo utaona kibao kinachoelekeza shule ilipo kutoka njia panda ya Samaksi kwenda shuleni ni kilometa 4 . Hapo kuna usafiri wa bodaboda hadi shuleni kwa gharama ya Tsh 2,000/= tu. Muhula wa masomo unaanza tarehe 14**/08/2023**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30.08.2023**
2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**.

**2.1 . SARE ZA SHULE DARASANI (WAVULANA)**

(a) Sare ya shule hii ni suruali mbili (02) light blue yenye rinda mbili kila upande pia iwe na upana usio chini ya inchi 18 (kumi na nane).
(b) Shati mbili (02) nyeupe za mikono mirefu zisizo na mchanganyiko wa rangi nyingine.
(c) Tai za light blue ndefu za kawaida mbili (02)
(d) Viatu jozi mbili (02) rangi nyeusi (visiwe na visigino virefu au buti) na viwe na kamba
(e) Soksi nyeusi
(f) Sweta rangi ya light blue
(g) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi na siyo wa tambi au inta.

**2.1.1 SARE ZA KUSHINDIA -WAVULANA (SHAMBA DRESS)**

(a) Suruali mbili (02) rangi ya nyeusi yenye rinda mbili kila upande, pia iwe na upana usio chini ya inchi 18 (kumi na nane).
(b) T-shirt dark blue yenye kola ambayo itapigwa mhuri shuleni
(c) Nguo za michezo (track suit, bukta, vyote viwe ni dark blue)
(d) Raba/njumu rangi yeyote

NB: **Mwanafunzi wakati wote awapo shuleni atapaswa kuvaa sare za shule tulizo agiza katika barua hii na sare ya bwenini, hivyo asije na nguo za nyumbani kwa sababu hazitopata muda wa kuvaliwa. Akikutwa na nguo za nyumbani katika sanduku au begi zitachukuliwa na hazitarudishwa na kupewa adhabu.**

### 2.2 MICHANGO YA SHULE.

a) Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi:-

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Kitambulisho | 5,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

***Angalizo : Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule*** A/C **Na.** ***42401100012*** *Jina la Akaunti* **NAISINYAI SECONDARY SCHOOL (NMB)** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip sawa na jina analotumia)

**"HAUTA POKELEWA ENDAPO HUTA KAMILISHA MAHITAJI YOTE MUHIMU YANAYOTAKIWA SHULENI"**

**b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Ream moja ya karatasi (A4) kwa mwaka kwaajili ya majaribio na mithani mbalimbali;
(ii) Godoro la sponji ($2^{1}/_{2}$ ft);
(iii) Shuka mbili rangi ya light blue,blanket,mto, taulo na chandarua.;
(iv) Ndoo moja (01) yenye mfuniko kwa matumizi binafsi.
(v) Daftari kubwa (quire three, four) 10
(viii)Vyombo vya chakula (kijiko,sahani,bakuli na vikombe) visiwe vya plastic
(ix) Kwanja (01), jembe (01) squizer (01) mfagio wa chelewa na hard broom.
(xii) Sanduku la chuma au bati lisiwe begi na uwe na kufuli mbili (02)
(xiii)Tochi/taa ndogo moja ya betri (itatumika iwapo umeme umekatika).
(xiv) Nakala ya cheti cha kuzaliwa au affidavity
(xiv) Njoo na vifaa vya usafi binafsi kama vile mswaki,dawa ya meno,mafuta, sabuni za kufulia na kuogea pamoja na kandambili za kuogea aina ya bata.
(xv) Njoo na kifaa cha kuhifadhia maji safi ya kunywa (dumu lita 5/3)
(xvi) Uje na vitabu vya masomo husika kulingana na tahasusi yako ulivyochaguliwa. Vitabu vya History, Geography, Kiswahili na General studies
(xvii) Uje na kadi ya BIMA ya afya au Kiasi cha shilingi 50400/= kukata Bima ya NHIF.

***NB*:** Ni muhimu ununue vitabu vyako mwenyewe kwa sababu shule haina vitabu vya kutosha kwa kila mwanafunzi. Ombi langu kwa wazazi/walezi kugharamia elimu ya mtoto wako kwa ubora wa elimu yake. Mzazi anaruhusiwa kuwasiliana na mwanae siku ya jumamosi na jumapili kuanzia saa kumi kamili hadi saa kumi na mbili jioni kwa kupitia namba za simu idara ya malezi 0787208688. Pia siku ya kutembelea wanafunzi ni kila jumapili ya mwisho wa mwezi.

## 3. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu, walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu, au mtu yeyote yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana;
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi au kukutwa na chaja ya simu katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau bendera ya taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xviii. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi.

**NB:** Endapo mwanafunzi atavunja kanuni/Sheria za Shule, atapewa adhabu moja wapo au zaidi ya zifuatazo:-

(a) Kuchapwa viboko visivyo zidi vinne kwa kila kosa
(b) Kufanya kazi ngumu
(c) Kupewa onyo la maandishi
(d) Kusimamishwa shule
(e) Kufukuzwa shule.

**4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical examination) ambayo itajazwa na mganga wa hospital ya serikali.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
(c) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu
(d) Orodha ya miongoni mwa vitabu ambavyo mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae miongoni mwake.

**KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI NAISINYAI**

THE HEADMASTER
NAISINYAI SECONDARY
SIMANJIRO - MANYARA

**WILLIAM J. OMBAY**
**MKUU WA SHULE**

**NB. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (Wizi kwa njia ya mitandao) baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa na watu wanaojitambulisha kama Walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ni mgonjwa na yuko maututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE , NI VYEMA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO :-**

1. **MKUU WA SHULE 0786023421**
2. **MAKAMU MKUU WA SHULE 0768711155**
3. **MWANDAMIZI TAALUMA 0692437560**
4. **MWANDAMIZI MALEZI 078720868**

**AHADI KWA SHULE**

AHADI NA UTII WA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE NIWAPO SHULENI

Mimi …………………………………………………………………………naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakao kuwa ninasoma hapa shuleni, kanuni na sheria zilizowekwa na Shule.

Sahihi ………………………………….                Tarehe …………………………

**Tanbihi ;**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyafanyia kazi kikamilifu

Namba ya simu ya mzazi au mlezi……………………………………………………

Jina la mzazi/mlezi…………………………….
Uhusiano ……………………………………...

Jina la mzazi/mlezi………………………………
Uhusiano: ………………………………………

Jina la mzazi/mlezi…………………………….
Uhusiano ……………………………………...

Jina la mzazi/mlezi………………………………
Uhusiano: ………………………………………

## SHULE YA SEKONDARI NAISINYAI

### HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi …………………………………… Dini /Dhehebu ……………….
2. Jina kamili la Baba ………………………………………………………………………
3. Je Baba yuko hai au amefariki …………………………………………………………
4. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ……………………………………..
5. Jina kamili la Mama ……………………………………………………………………
6. Je mama yuko hai au amefariki ………………………………………………………..
7. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ……………………………………..
8. Anuani ya Mzazi ……………………………………………

   S.L.P ………………………………………..

9. Kazi ya Baba ………………………………………………………………………………
10. Sehemu anayofanyia kazi ………………………………………………………………..
11. Kazi aifanyayo Mama ……………………………………………………………………
12. Sehemu anakofanyia kazi ………………………………………………………………
13. Kama huishi na Mzazi wako taja jina la Mlezi wako …………………………………
14. Kazi aifanyayo………………………………………………………………………………
15. Sehemu anakofanyia kazi ………………………………………………………………
16. Anuani ya Mlezi ………………………………………………………

    S.L.P ………………………………………………

17. Habari nyingine za familia ;

| Jina la Kaka / Dada | Umri | kazi yake | Mahali anapofanyia kazi Kama ni mwanafinzi taja Shule. |
|---|---|---|---|
| (a) ……………………… | ……… | …………….. | ……………………………… |
| (b) ……………………… | …….. | ……………. | ……………………………… |

18. Afya ya Mwanafunzi (Tafadhali eleza kama una ugonjwa wowote ambao una kukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu) Ni muhimu umfahamishe Daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayomuhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu.

    ………………………………………………………………………………………………………

    ………………………………………………………………………………………………
19. Uthibitisho wa Mwanafunzi;

    Nathibitisha kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.

    Sahihi ………………………………………………………………………………

    Tarehe ………………………………………………………………………………

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY KIGOMA

NAISINYAI SECONDARY SCHOOL.

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

(To be completed by a Medical officer in respect of all form Entrance)

Pupil's full name ……………………………………………………………………………………………

Age …………………………. (Year) …………………………. Sex …………………… ……………………

Stool examination ………………………………………………………………………………………

Urinalysis ………………………………………………………………………………………………

Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………………

Syphilis Test ……………………………………………………………………………………………

T.B Test …………………………………………………………………………………………………

Eye Test …………………………………………………………………………………………………

Skin ……………………………………………………………………………………………………

Spleen …………………………………………………………………………………………………

Abdomen …………………………………………………………………………………………………

Additional information eg. Physical defect or impairment(s), chronic infections or family diseases

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above pupil and recommend that he/she is fit/ unfit to pursue further education

Signed ……………………………………………………………………………………

Designation ……………………………………………………………………………

Official Stamp:

Date: …………………………………

(Delete whichever is in applicable)

## ORODHA YA VITABU MUHIMU UNAVYOPASWA KUWA NAVYO KAMA UNAWEZA KUJINUNULIA.

### A-LEVEL HISTORY I


1. Illife,J.(1995). Africans, the History of the continent. Edinburg, Cambridge; university press, London UK.

2. Manning, P.(1990).Slavery and African life; occidental oriental and African slave trade, Cambridge University Press.

3. Njiro, E.(1989). A History of Africa in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.

4. Rodney, W.(1989). How Europe underdeveloped Africa, publishing House, Dar es salaam, Tanzania

5. Shillington, K.(2004).History of Africa. Macmillan publishers. Hong, japan

6. Davidson, E. ef al (1997); The growth of the African civilization East and central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore

7. Freud, B.(1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.

8. Kimambo, I and Temu, A(1969); A history of Tanzania, East Africa publishing House Nairobi, Kenya

9. Robin, H.(1993); African since 1875 1872 A modern History, East African Publishers ltd, Nairobi, Kenya

10. Roland, O. and Anthony, A.(2007).Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.

11. History for secondary schools form five (Tanzania Institute of Education)

12. History for secondary schools form six (Tanzania Institute of Education)

13. History for secondary schools: from five (TIE)

14. History for secondary schools: form six (TIE)


### A-LEVEL HISTORY II


1. Nelson throne Essential modern world history

2. History of 21st century (World history)-Oxford

3. H.L. Peacock. (2010).A History of modern Europe 1789-1981. Seventh Edition

4. The History of Modern World. (2007). 6th Edition. Oxford University press

**GEOGRAPHY**

1. Physical Geography by D.T Msabila
2. Geography in Diagrams for Africa by R.B. Bunett
3. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard
4. Human & Economic Geography (Advanced level paper 2) by D.T Msabila
5. Map Reading for East Africa by D. N. McMaster
6. Practical Geography (Map, Photo, statistics, survey& Research) for A. Level by Zisti Kamili

**ALEVELKISWAHILI**

**1.VITABU VYA UCHAMBUZI**

**USHAIRI**

Kimbunga-H.Goro Edition.OxfordUniversitypress

**RIWAYA**

- Fungateyauhuru–M.S.Khatibu
- Chungutamu–T.A.Mvungi
- Vutan`kuvute–S.AShafi
- Usikuutakapokwisha–M.Msokile
- Mfadhili–H.Tuwa

**TAMTHILIYA**

- MORANI–E.Mbogo
- Nguzomama–P.Mohamedi

2.Kiswahilisekondari–kidatochaV&VI-Oxford
3.Kiswahilisekondari–kidatochaTano(TIE)
4.Kiswahilisekondari–kidatochasita(TIE)

**A-LEVEL GENERALSTUDIES**

- UNDERSTANDINGADVANCEDLEVELGENERALSTUDY
- ADVANCEDLEVELSECONDARYSCHOOLEDUCATION byJoannesandSospeterM. Deogratias
- GENERALSTUDIESPAPERREVIEW,,any of recent years.
- RICHARD,r.f.Mbalase.General Studies for Advancedlevelcertificate
- Mgaywa,B.M.GeneralstudiesforAdvancedlevel3rdEd.
- Joannes Brigiwa Mungu&Sospeter.M.Deogratıes.Understanding Advanced level General studies;Advanced Secondary school Education